NI NANI HUYU?

Ubarikiwe, ndugu. Inapendeza sana kufika katika nyumba ya Bwana.

2 Nafikiri nilikuwa nikisoma Maandiko fulani, siku moja, nayo yalisema ya kwamba Yesu alipokaribia Yerusalemu, ya kwamba wanafunzi waliinua macho yao wakauona mji mtakatifu kwa mbali, nao wakaanza kushangilia na kusema, ya kwamba, "Sasa ufalme utarudishwa."

3 Naye mtu huyu fulani aliyekuwa akisimulia, ama kuzungumza juu ya ziara ya hivi majuzi ya Palestina, naye akasema ya kwamba watu sasa, katika mwaka uliopita, wamekuwa wakija mahali ambapo, wanapopanda kutoka bondeni na kutazama kwenye kona, njia ile ile ambayo Yesu na wanafunzi walipitia wakati huo, ya kwamba wanapouona huo mji, wanaanza kulia.

4 Mnajua, ninaamini, kulikuwa na jambo fulani hao wanafunzi, katika siku hizo, walihisi, ya kwamba—ya kwamba ufalme ungerudishwa tena.

5 Na sasa wakati u karibu sana. Nami naamini hiyo ndiyo hisia iliyo juu ya watu, ya kwamba ufalme uko karibu sana kurudishwa tena.

6 Ndugu Neville, mchungaji wetu wa thamani na mbarikiwa, amezungumza nami hivi punde kuhusu jitihada za ufufuo unaokuja hapa maskanini, katika siku chache usiku, tuwe tukiuombea. Ndipo nikamwambia, nilifikiri lingekuwa jambo la heri.

7 Kamwe huwezi kuwa na ufufuo mwingi kupita kiasi. Na mara nyingi tunapata maoni yasiyo sahihi ya uamsho. Uamsho sana sana sio kuwaleta wafuasi wapya, lakini ni kufufua wale tulio nao tayari. Na mimi . . .

8 Ninapenda kusema hivi, kwa sababu ninalisema kutoka kwenye kilindi cha moyo wangu. Kwamba nimeanza kupata hisia tofauti huku maskanini kuliko ile ambayo imekuwako kwa muda mrefu, hisia ya—ya kina cha kiroho, kama vile ilivyokuwa, zamani za kale; kile kifu fulani ambacho hutulia, na kina msingi halisi. Nami natumaini ya kwamba Mungu atalibariki kanisa hili dogo, na . . .?. . . tena katika nguvu zake.

9 Nami ninaona mradi wa ujenzi ukiendelea, na ninadhani hilo ni jambo zuri sana. Kwa maana, hapana budi, sisi wazee tutavua silaha na kuzirudisha mikononi mwa watoto wetu, na kupanda vile Vipandio vya dhahabu.

10 Hivi majuzi nilipita ile alama ya nusu-ya safari sasa, ya umri wa miaka hamsini. Kamwe siwezi kutambua hilo. Haionekani

kama umekuwa muda wowote tangu nilipokuwa nikisafirisha mboga za Chris Meisner, nikiwa na yapata umri wa miaka kumi na minane, kumi na sita, kumi na minane. Lakini ikaenda tu mahali fulani. Inaonyesha tu ya kwamba hapa hatuna mji udumuo, bali twautafuta Ule ujao. Na huo ndio Mji ambao Mungu ndiye mjenzi, na hakutakuwako na mwisho kule.

11 Asubuhi ya leo, nilipokuwa nikizungumza juu ya somo la Siku ya Mama, na kujaribu kumweka mama si jinsi alivyo hasa, katika uzee, akiwa na makunyanzi, na yote haya, mikongojo yake, au kiti cha magurudumu kikuukuu, ama kiti cha mkono, na chungu kidogo cha maua kimewekwa karibu naye; bali mama katika ufufuo, amerudishwa katika ujana wake, na amesimama, aking'aa kama malkia. Hivyo ndivyo ninavyopenda kumwazia mama yangu. Sipendi kumwazia kama alivyo leo hii, mkongwe. Ninapenda kuwazia yajayo. Nami najua mnajisikia hivyo kuhusu mama zenu. Mwazie jinsi alivyo hasa moyoni mwake. Ingawa wengi . . . kama mshairi asemavyo, "Maisha hayajakuwa rahisi kwake, lakini angeyaishi yote tena, ili tu akufanyie jambo fulani." Kwa hivyo Mungu atafanya njia ili aweze kuishi milele pamoja na wewe. Kwa hivyo ninafurahia hilo.

12 Sijui ni kwa nini, nilitoa tangazo hili, asubuhi ya leo, kwamba ningezungumza usiku wa leo, Bwana akipenda, juu ya: *Ni Nani Huyu?* Hakika sijui jinsi nitakavyolifanya. Lakini nimekuwa na shughuli nyingi hadi yapata saa moja na dakika kumi zilizopita, kwenye mahojiano alasiri nzima, pia nilikuwa na simu maalum na—na za dharura. Nisingeweza kuzitimiza.

13 Nami nawatakeni mwendelee kumuombea Daktari Sam. A—anapata nafuu vizuri, nasi tunashukuru. Naye Daktari Baldwin na Bibi Baldwin wote wanaendelea kupata nafuu. Wanaendelea vizuri.

14 Ninawatakeni muweke mmoja mpya kwenye orodha yenu ya maombi, alasiri ya leo. Huyo ni Harry Lease hapa chini, muuza dawa. Harry ni rafiki yangu binafsi. Na muda wote ambao nimemjua, nilifikiri alikuwa Mkristo, mpaka alasiri hii, wakati ndugu yake alipoleta haja kwa ajili ya wokovu wa nafsi yake. Ndugu Mike Egan alileta . . . mdhamini wetu hapa, alileta hizo habari. Naye Harry ni mahututi, huko hospitalini. Sikujua aliniwazia kiasi hicho; lakini, alimkatalia mbali mchungaji wake mwenyewe, alasiri ya leo, au mchungaji wa kanisa ambako yeye huenda, naye akanitaka nije nikamwone. Nami ninataka kwenda kumwona. Kwa hiyo, mwombeeni Harry.

15 Tuna furaha hapa, usiku wa leo, kutambua, kuna marafiki zangu hapa, kutoka huko chini Georgia, Ndugu Welch Evans na familia yake. Ninaona, pia, wageni wengine ambao sikuwafahamu, labda walikuwa hapa asubuhi ya leo.

16 Kama sijakosea, ninamwona Ndugu na Dada Elmer Collins kule nyuma, kutoka Phoenix, Arizona. Loo, hujabadilika.

Inaonekana kana kwamba unapaswa kuwa na nguo zako za reli, na—na ukija kutoka kwenye njia ya reli. Basi karibu tena nyumbani! Siwezi kukuomba ukae huku, maana umepata mahali pazuri zaidi, unaona, ambapo ni pazuri sana, Phoenix. Ningependa kuishi huko, siku moja, mimi mwenyewe.

17 Na halafu ninamwona Ndugu Smith hapa, wa Church of God, huko nje. Ndugu Smith, nilipewa, kitabu chako kidogo, hivi majuzi, ama jana alasiri, kuchelewa. Bado sijakisoma, lakini bila shaka nitakiidhinisha, mradi tu najua ulikiandika. Hakina budi kuwa ni halisi, Maandiko ya kweli. Mungu akubariki. Nami natumaini kitafanikiwa.

18 Na wengine wengi, ningeweza kusema. Nyote mmekaribishwa hapa maskanini. Nami niliufurahia wimbo ule, asubuhi ya leo, wa Dada Stricker aliyeimba, "Anamtazama, yeye, kupitia kwenye tundu." Ndugu zangu Wamenoni hapa, nina furaha kuwa nao humu. Na, loo, ninyi nyote! Rafiki mmoja hapa, ninaamini, kutoka huko Illinois, mwanawe anarekodi sauti huko nyuma, nitakutana nao tena. Na wengi sana, naweza . . . Usifikiri kwamba ninakudharau ikiwa sitalitaja jina lako, lakini nawakaribisha tu ninyi nyote.

19 Sasa hebu tusome usiku wa leo, kwa ajili ya funzo la Maandiko, kutoka katika Mathayo mlango wa 21, kuanzia kifungu cha kwanza, na kusoma chini, na cha 11, vyote pamoja.

> *Hata walipokaribia Yerusalemu,* kukaja, na kufika *Bethfage, katika mlima wa* Mizeituni, *ndipo Yesu alipowatuma wanafunzi wawili,*
>
> *Akawaambia, Enendeni mpaka kijiji kile kinachowakabili, na mara mtaona punda amefungwa, na mwana-punda pamoja naye:* wa*fungueni, mniletee.*
>
> *Na kama mtu akiwaambieni neno, semeni, Bwana anawahitaji; na mara huyo atawapeleka.*
>
> *Hayo yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema,*
>
> *Mwambieni . . .* binti *Sayuni, Tazama, Mfalme wako anakuja kwako,* mpole . . . *amepanda punda, na mwana-punda, mtoto wa punda.*
>
> *Wale wanafunzi wakaenda, wakafanya kama Yesu alivyowaamuru,*
>
> *Wakamleta yule punda na mwana-punda, wakaweka nguo zao juu yao, wakampandisha juu yake.*
>
> *Ndipo umati mkubwa sana ukatandaza mavazi yao njiani;* nao *wakakata matawi ya miti,* wakayatandaza *njiani.*
>
> *Na* makutano *waliotangulia, na wale waliofuata, wakapaza sauti, wakisema, Hosana, Mwana wa Daudi:*

Ndiye mbarikiwa yeye ajaye kwa jina la Bwana; Hosana juu mbinguni.

Hata alipoingia Yerusalemu, mji wote ukataharuki, watu wakisema, Ni nani huyu?

Nao makutano wakasema, Huyu ni Yesu, yule nabii wa Nazareti . . .

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa maombi.

20 Ee Bwana, tunashangaa tu tungesema nini, kama tungaliishi katika siku hizo. Lakini tunaishi katika siku kuu zaidi, tunapomtazamia Yeye kuja. Na tunapofanya maandalizi, Bwana, tukiitayarisha mioyo yetu, na kuleta miganda yote tunayoweza kukusanya kutoka kwenye mashamba ya mavuno, nyumbani na nchi za ng'ambo pia, tunawazia na katika kuutazamia wakati ule tutakapomwona Yeye akija, amepanda farasi mweupe, akishuka kutoka kwenye malango ya Utukufuni, kuibadili na kuitengeneza maskini miili hii yetu iharibikayo, iwe mwili wenye utukufu kama Wake, ambapo hapawezi kuwa na dhambi au hakuna dalili ya mauti kuingia. Nasi tutamwona jinsi alivyo, na kuishi, na kumpenda katika nyakati zote zijazo.

21 Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya kanisa hili na kwa ajili ya mchungaji wake, na kwa ajili ya wadhamini na mashemasi, na kwa ajili ya kila mtu anayekuja hapa; na kwa ajili ya wageni walio malangoni petu, ambao ni kondoo wa zizi lile lile, lakini kutoka boma lingine. Tungeomba ya kwamba ungewabariki, usiku wa leo, kwa Uwepo Wako.

22 Na utulishe Neno Lako, ili tuweze kutoka hapa, usiku wa leo, tukiwa na azimio la kuwa Wakristo bora kuliko tulivyowahi kuwa. Jalia twende na tumaini jipya mioyoni mwetu, pamoja na shangwe, tukikungojea Kuja Kwake.

23 Ikiwa kunaweza kuwako na wengine miongoni mwetu, walio wagonjwa na wanaoteseka, tusingesahau kuwaombea. Kwamba wao . . . Wakiingia kwenye jengo, usiku wa leo, ambamo tumekusanyika kwa ajili ya ibada, wakiingia, wagonjwa, jalia waondoke wakiwa wazima.

24 Pia tungewaombea wale wanaopata ahueni, manyumbani na hospitalini, nao wako kwenye vitanda vya mateso. Tunaomba, Ee Mungu, kwamba rehema Zako zitawashukia.

25 Tungewaombea wale wasiojali, usiku wa leo, ambao bado hawajaonja na kuona Bwana yu mwema, wasiojua maana ya kupendwa na Mungu. Kamwe hawaelewi wanayokosa. Ee Mungu, jalia matangazo fulani ya redio, au kwa njia fulani, iguse mioyo yao, na mihemko yao ielekezwe Kwako kabla mlango wa rehema haujafungwa na wakafungiwa nje, ili kustahimili hukumu pasipo na rehema.

26 Tusaidie, Bwana. Mambo haya tunaomba katika Jina la Bwana Yesu, na kwa ajili ya utukufu Wake tunaomba. Amina.

27 Watu walikuwa wamesongamana sana malangoni, nayo mitaa ilijaa watu, wala hata hapakuwapo na nafasi ya watu kulala. Walikuwa wamelala nje ya ukuta, kila mahali, kwa sababu hii ilikuwa ni pasaka. Na watu walikuja kutoka kote katika ulimwengu unaojulikana, kuabudu wakati huu. Ulikuwa ni wakati ambapo mwana-kondoo wa pasaka alichinjwa. Na . . . Uliwakilisha ukombozi wao kutoka Misri, ule utumwa. Na waliadhimisha hii, kila mwaka. Kila mwaka, pasaka hii kuu ilifanyika. Basi ulikuwa mmoja wa nyakati bora zaidi za . . . au matukio ya dini ya Kiyahudi, kwa sababu ulimaanisha ule wakati waliokombolewa.

28 Watu wote wanapenda kuuwazia huo, wakati waliokombolewa. Jinsi ambavyo kila mmoja wetu, usiku wa leo, anaweza kurudi kwenye wakati tuliokombolewa! Ulichomaanisha kwetu!

29 Ninaweza kukumbuka katika ujuzi wangu mwenyewe, jinsi maskini moyo wangu wa ujana ulivyotamani sana kumgusa Mungu. Niliwazia, "Loo, laiti ningaliweza tu kupanda juu na kubisha mlangoni Pake, na kuzungumza Naye kidogo!" Na, bila shaka, mnaijua hadithi yangu. Nilijichukulia karatasi na penseli, nami nilitaka kumwandikia barua, maana singeweza kuzungumza Naye. Nami nilijua ya kwamba Yeye aliishi msituni, kwa sababu nilikuwa nimemsikia, pia nilikuwa nimeyaona matendo Yake msituni. Na nji—njia fulani ya kale ya miguu, niliyozoea kupitia wakati nikiwinda au nikienda kuvua samaki. Niliwazia, "Nitaitundika tu mtini, na anwani iwe ni kwa Bw. Yesu." Njia fulani tu kusudi mzigo huo uweze kuondoka moyoni mwangu.

30 Loo, usiku huo, kule chini! Ninaweza nikasahau umri wangu, naweza hata kusahau jina langu siku moja, ila siwezi kusahau saa ile aliponikomboa kutoka katika dhambi. Jambo fulani lilifanyika, chini ndani yangu, ambacho kimenisaidia kupitia majira makuu katika giza. Ile saa ya ukombozi wangu, mizigo ya dhambi iliniondokea, ndipo nikawa mtu mpya. Nimekuwa kiumbe kipya katika Kristo Yesu, tangu wakati huo.

31 Nao Wayahudi hawa, walikuja, kila mwaka. Na kulikuwa na che—chemchemi ndani ya kanisa. Nao wakala m—mkate, na mboga zenye uchungu, na mwana-kondoo, nao wakainywea chemchemi hii kanisani. Nao wakafurahi pamoja kwa sababu Mungu alikuwa amewafadhili. Kwa hiyo, huu ukiwa ni wakati wa pasaka, wala haikuwa tu ni pasaka, bali ilikuwa ni pasaka maalum.

32 Mnajua, kuna wakati mwingine ambao tunaenda kanisani na . . . Sikuzote tunapenda kwenda, lakini kuna nyakati zingine ambapo kitu fulani maalum hutokea.

33 Nao huu ulikuwa ni mmoja wa nyakati hizo. Hewa ilikuwa imejaa matarajio, kama tu ilivyo leo hii. Macho yote ya wale waliompenda yalimtazamia aingie langoni.

34 Nami naamini zaidi sana ndivyo ilivyo leo, kwa kuwa wale wanaompenda wanamtazamia. Hewa imejaa matarajio.

35 Wakati, tunaishi katika siku hii, ambapo dunia kwa kweli, imekuwa pipa moja kubwa la baruti. Nayo sayansi inatuambia, "Bado dakika tatu tu ifike usiku wa manane." Nami nina hakika mlikuwa mkisoma, kama mimi, hivi majuzi, ile hadithi ya jenerali huyu katika jeshi, alisema, kwamba, "Kama kungekuwa na vita vingine, vingechukua tu dakika mbili au tatu." Siku za kale za vita, na kufyatua bunduki, na kuchimba mahandaki, hizo zote zimekwisha. Wanadai vita vijavyo vitachukua tu dakika mbili au tatu. Siku moja, mtu fulani aliyechanganyikiwa kabisa atafunua kifuniko chake na kurusha moja ya hayo mabomu. Nao watakapofanya hivyo, tunavyo vilindo vya ujasusi, kila mahali, kuyarusha moja kwa moja tena. Dunia kamwe haiwezi kustahimili hayo.

36 Kila mtu kwenye hiyo pasaka alijua jambo fulani lilikuwa linaenda kutukia, lakini hawakujua lilikuwa ni nini hasa.

37 Na hivyo ndivyo ilivyo leo. Karibu kila mtu anajua kwamba jambo fulani linakaribia kutokea. Kila mtu anajua hilo. Unaweza kuzungumza na mwenye dhambi, unaweza kuzungumza na mfanyabiashara, unaweza kuzungumza na mtu yeyote, na, loo, ni wakati usio na utulivu sana kwa ulimwengu.

38 Lakini unaweza kuzungumza na mwanamume ama mwanamke anayemtazamia Yeye kuja, nao utukufu uko usoni mwao, ukiangaza. Wanalitazamia tukio hilo kuu. Kwa hiyo hewa yote imetaharuki tena, ikitarajia jambo fulani kutukia. Ulimwengu haujui kinachokaribia kutukia, lakini Kanisa la Mungu aliye hai linajua kitakachotukia. Wanajua ya kwamba hivi karibuni baragumu italia, nasi tutamwona Yeye akija, kutoka Utukufuni, amepanda farasi mweupe, nayo majeshi ya Mbinguni yakimfuata. Nao wale waliokufa katika Kristo watanyakuliwa na kutwaliwa juu ili kumlaki hewani. Hicho ndicho tunachotazamia. Tunakitamani.

39 Nasi tunaambiwa ya kwamba nafsi za akina mama hao, na kadhalika, tulizozungumza habari zake asubuhi ya leo, chini tu ya madhabahu ya Mungu, zinapaza sauti, "Hata lini, Bwana? Hata lini?" Mama anataka kukuona kadiri unavyotaka kumwona. Nao wapendwa wetu wanataka kukutana nasi kadiri tunavyotaka kukutana nao.

40 Huo utakuwa ni muungano wa namna gani, hapo atakapokuja! Kukutana na wapendwa wetu na kuwaona katika mwili wao wa ufufuo, na uliotukuzwa, na kutembea pamoja na mrithi wa ufufuo, tukiangalia tabia zao, jinsi zimebadilika, upole na utulivu. Na haitakuwa ni mkukumkuku na kurukaruka

na mishtuo, kwa maana tutakuwa na Umilele wote kuishi pamoja.

41 Loo, wakati huu mkuu wa ukichaa tunaoishi, kamwe si wakati wa chochote, kupanda tu, na kugutuka, na kunyakua, mbona, ni siku ya kuchukiza sana.

42 Kisha, walipokuwa wakingojea jambo fulani litokee, ilikuwa ni vibaya sana kwamba wengi wa wale waliokuwa kwenye pasaka kamwe hawakupata kumwona. Hata hivyo, walijua jambo fulani lilikuwa linaenda kutukia, lakini hata hivyo hawakupata kumwona.

43 Ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwa Bwana. Kuna watu wengi wasiotulia, siku hizi, wanaojua ya kwamba jambo fulani liko karibu kutukia, lakini kamwe ha—hawatamwona. Kwa maana atakuja katika utulivu wa usiku wa manane, kulinyakua Kanisa hilo dogo ambalo linatamani na kungoja na kutarajia kumwona. Hao ndio atakuja na kuwachukua. Wengi wa ulimwengu ambao wanaishi kwa madoido, na kuzilisha nafsi zao vitu vya ulimwengu, kamwe hawatajua kilichotokea, mpaka Kanisa litakapoingia Utukufuni, kwa maana Yeye atakuja kama mwivi usiku na kuwachukua. Kwa hivyo tunaweza kuona tumerudi tena mahali pale pale. Sasa tunaona, ya kwamba, matarajio haya, ya kwamba Mungu huwajia wale ambao . . . Kote katika Maandiko, limekuwa ni jambo lile lile. Kwamba wao ni . . . Yeye daima huwatokea wale wanaomtarajia, daima kwa wale wanaotaka kumwona. Nami nina hakika ya kwamba hilo ndilo tumaini lililo mioyoni mwetu usiku wa leo.

44 Imekuwa kama miezi sita iliyopita, nadhani, nilikuwa nikitoa ushuhuda kwa watu fulani. Nami nikasema, "Loo, kuliwazia, ya kwamba wakati wowote Yeye atakuja!"

45 Na kilichonifanya niseme hivyo, nilikuwa nikizungumza juu ya Ndugu Bosworth. Nilipoenda kumwona mtakatifu huyo mkongwe, tuliposikia alikuwa yuafa, umri wa miaka themanini na kitu, mimi na mke wangu tukishuka huko . . . huko kumwona kabla hajafa. Ilibidi tu nimwambie jambo fulani. Ninapenda kuwatazama watakatifu wanapoingia Utukufuni, na ilinibidi kumwona. Ndipo tukaendesha gari kwa kasi sana.

46 Lakini nilipofika kule, na kukimbilia mlangoni, kwenye kona ndogo alilala maskini huyo mzee wetu. Aliinua kichwa chake aliponiona nikija. Mikono yake mizee, iliyodhoofika ikining'inia nje, huku nyama ikining'inia chini. Naye akaninyoshea mikono yake. Ndipo nikamkumbatia shingoni na kupaza sauti, "Baba yangu, baba yangu, magari ya Israeli, na wapanda farasi wake," kwa maana alikuwa mtu mtakatifu, mtauwa.

47 Ndipo nikasema, "Ndugu Bosworth, ninataka kukuuliza jambo fulani. Je, unaamini kwamba utakuwa mzima?"

Akasema, "Loo, mimi hata si mgonjwa."

Nikasema, "Vema, kuna shida gani?"

48 Akasema, "Ninaenda Nyumbani." Akasema, "Nimechoka, na nimedhoofika. Nami ninataka tu kwenda Nyumbani."

49 Nikasema, "Basi unatambua kuwa unakufa?" Nikasema, "Nataka kukuuliza jambo fulani. Huko nyuma katika miaka sabini na kitu ya huduma, dakika yako tukufu zaidi imekuwa ni ipi? Naomba uongee nami, bwana, na kuniambia ni tukio lipi ulilokuwa nalo, safarini, ambalo ungeweza kulihesabu ni saa yako iliyo kuu kuliko zote."

50 Nikiishi kuuona umri wake, kamwe nisingeweza kusahau, wakati macho hayo meusi yaliponiangalia, juu ya miwani hiyo. Akasema, "Ndugu yangu mpendwa, huu ndio wakati mkuu zaidi wa maisha yangu. Siwezi kuwazia wakati wowote ambao ulikuwa mtukufu kuliko sasa hivi."

51 Nikamtazama usoni, nikasema, "Bwana, bado ungali unajua kuwa unakufa?"

52 Akasema, "Ndugu Branham, nimelala hapa, nikingojea kila dakika Yeye aufungue mlango huo aje, anipeleke Nyumbani pamoja Naye." Hiyo ndiyo njia ya kufa. Hiyo ndiyo njia ya kuondoka.

53 Na kama mjuavyo, kwamba, yapata saa mbili kabla hajafa . . . Alikuwa, alikuwa amekosa fahamu, kwa zaidi ya siku mbili. Ndipo alipojirudia, alisimama humo chumbani, akaanza kuzungumza na mke wake. Ndipo, kwa ghafla, alionekana kuwa mwangavu. Naye akapeana mikono, kwa saa nzima au zaidi, na marafiki, ambao wamekufa kwa miaka arobaini au hamsini, waliokuwa waongofu wake kanisani mwake. Akapeana mikono na mama yake na baba yake. Mpaka alipokuwa . . . uhai ulipokuwa umeuacha mwili wake, akajilaza juu ya mto akalala, mikononi mwa Bwana Yesu. Hakuna kitu kama kumtumikia Yeye, kumtarajia.

54 Basi nilipokuwa nikizungumza na mtu huyu kuhusu jambo hili, na kusimulia tukio hilo, nilisema jambo hili. Nikasema, "Bwana, loo, si itakuwa tukufu tutakapomwona? Loo, laiti angalikuja leo!"

Akasema, "Ndugu Branham, usiwaogopeshe watu namna hiyo."

Nikasema, "Unamaanisha nini?"

55 Akasema, "Loo, usijaribu kuwaambia watu kwamba ulimwengu unakuja, au Kristo anakuja. Inawatia hofu."

56 "Loo," nikasema, "la. Samahani. Kwa wale wanaomtazamia, ndizo habari tukufu zaidi ambazo wangeweza kusikia, kwamba Yesu yu karibu sana kutokea na kulichukua Kanisa Lake." Uzee utabadilishwa uwe ujana. Furaha itatolewa badala ya majonzi. Uhai utatolewa badala ya mauti. Kutokupatikana na mauti

kutabadilishwa, na maadili. Loo, ni wakati wa namna gani, kujua ya kwamba Yeye atakuja!

57 Walikuwa wakimtazamia. Walikuwa wakimtarajia. Naye alipokuja, tuliona ya kwamba kulikuwa na makundi mawili. Kundi moja lilisimama na Yeye, na moja lilikuwa likimpinga.

58 Na hivyo ndivyo tunavyoiona leo. Hivyo ndivyo, kuja Kwake, daima kumewagawanya watu. Kila wakati, unapomkuta Yesu, unawakuta hapo wale ambao wanampinga. Huyo ni Shetani. Na, leo hii, tunapoliwazia, hatuoni mabadiliko mengi. Vile vile tu. Watu wamebadilika, bali roho ya watu haijabadilika.

59 Kwa hiyo hatimaye walipotazama nje ya lango na kumwona akija, amepanda maskini yule punda mdogo, mweupe, si ajabu wanafunzi walianza ku—kupiga mayowe, "Ufalme wa Mbinguni umekuja!" Watu wakakimbia kumlaki, na Yerusalemu nzima ikataharuki. Kuna kitu juu yake, Yesu anapokuja, daima ni taharuki. Nao mji wote ukataharuki. Wala ha—hawawezi kulificha.

60 Basi iliwabidi wahubiri wa siku hiyo kutoa hesabu kwa ajili ya taharuki hii, kwa sababu ilikuwa kwenye sikukuu ya pasaka. Nao wakapaza sauti, "Ni nani Huyu?" wakati hewa ilipojaa taharuki, nako kuja kwa Bwana Yesu, Yerusalemu, kulikuwa kumeijaza sana hewa kwa matarajio, inaonekana waalimu walipaswa kujua litakalotukia. Ilionekana kana kwamba kuhani mkuu angelijua hilo. Ilionekana kana kwamba makuhani wengine wote wangelijua hilo.

61 Wala halijabadilika hata kidogo, leo hii, kwa sababu Roho Mtakatifu anakutangulia Kuja kwa Bwana Yesu. Naye Roho Mtakatifu anapoanza kuenea kote duniani, mioto ya uamsho inazuka, kila mahali, ishara kuu na maajabu yamefanywa, uponyaji umetukia, unabii umetolewa. Mkusanyiko wote wa baraka za kimitume umerudi tena Kanisani. Basi, kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo sasa, roho ya asiyeamini ingali inapaza sauti, "Ni nani Huyu?"

62 Baadhi yao walimwamini Bwana Yesu, kusema Yeye alikuwa Mtu mwema. Baadhi yao walisema, "Yeye ni Mtu mwema."

63 Ndivyo wanavyosema siku hizi. Wanajaribu kumweka kama Napoleon, shujaa. Wanajaribu kumweka kama Ge—George Washington, mtu mkweli. Lakini Yeye alikuwa zaidi ya hayo.

64 Je, uliona usomaji wa Maandiko? Wao walisema, "Huyu ni Nabii anayetoka Galilaya."

65 Nao wanajaribu kusema jambo lile lile siku hizi, wanapoyaona matendo haya makuu ya Bwana: kuwapa tena, afya, wagonjwa na wanaoteseka; kumwona akimtumia Roho Wake Kanisani Mwake, kuyapambanua mawazo ya watu; kumwona akifanya kama tu alivyofanya alipokuwa hapa

duniani, kutimiza yale aliyosema yangetukia; bila shaka, makanisa na watu wameuliza, hivi, "Ni nani Huyu?"

66 Hawakuelewa Yesu alikuwa ni nani, kwa sababu hakuna hata mmoja wao angeweza kumtambua, kwa shule zao. "Alitoka katika seminari gani? Alitoka shule gani ya theolojia?"

67 Basi ndivyo ilivyo siku hizi. Wengi wa watu waliotiwa mafuta na Roho Mtakatifu hawakutoka kwenye seminari yoyote. Ni matokeo ya chaguo la Mungu mwenyewe. Lakini ishara na miujiza, na maajabu yaliyoahidiwa katika Biblia, hufuatana na huyu Roho Mtakatifu mkuu anapotenda kazi miongoni mwa watu.

68 Nao wanasema siku hizi, "Kwani wanatoka shule gani?" Mara tu unapoingia kwenye mji, kufanya uamsho, "Je, wewe ni wa dhehebu gani?"

69 Nilikuwa na mahojiano Ijumaa alasiri, pamoja na kasisi wa Katoliki ya Kirumi kutoka kanisa la Kiairishi huko Louisville. Na mara nilipotambulishwa kwake, mwanachuoni hodari, alisema, "Bw. Branham, uko na dhehebu gani?"

Nikasema, "Siko na lolote."

Naye akasema, basi, "Je, uliwekwa wakfu?"

Nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Ni nani aliyekuweka wakfu?"

70 Nikasema, "Bwana Yesu alinipa Roho Mtakatifu, kuihubiri Injili, kisha akanipa agizo." Vema, hilo ndilo agizo tunalohitaji.

71 Yesu kamwe hakuwaambia wanafunzi Wake, "Enendeni kwa . . . " Siyakosoi mambo hayo, lakini yametimiza siku yao. Yeye hakusema, "Nenda, ukasome uwe mhudumu, kwa miaka *kadhaa*."

72 Alisema, "Ngojeni katika mji wa Yerusalemu, mpaka mtakapovikwa Uwezo utokao Juu." Alisema hayo kwa watu ambao wasingeweza kuandika majina yao wenyewe. "Na baada ya huyu, Roho Mtakatifu akisha kuwajilia, ndipo mtakuwa mashahidi Wangu, katika Yerusalemu, Uyahudi, Samaria, na hata sehemu za mwisho za dunia pia." Hilo ndilo agizo.

73 Kamwe hatuna kumbukumbu ya Yesu akienda kwenye shule yoyote, wala kuhitimu kutoka seminari yoyote. Hata hivyo, kumekuwa na seminari nyingi zaidi zilizojengwa kwa Jina Lake, kwa sababu za kidini, kuliko kitu—kitu kingine chochote ambacho kimewahi kuwepo duniani. Hatukuwahi kuwa na kumbukumbu yo—yoyote Yake kwenda shuleni kamwe. Lakini, hata hivyo, kumekuwako na shule nyingi zaidi zilizojengwa kwa Jina Lake kuliko kwa jina lingine lolote chini ya mbingu, shule. Hatukuwahi kujua Yeye akiandika kitabu. Hata hivyo, kumekuwako na vitabu vingi sana vilivyoandikwa kumhusu Yeye kuliko vitabu vingine vyote ambavyo vimeandikwa. Na,

siku hizi, Biblia Yake ndiyo Kitabu maarufu kuliko vyote kilichopo ulimwenguni mwote, miongoni mwa vitabu vyote.

74 Lakini, mnaona, katika siku ile ya kuzuriwa, wao walipaza sauti, "Yu nani Yeye?"

75 Mnaona, Mungu huchukua kitu kinachoonekana kana kwamba si kitu, kufanya kitu kutoka kwake. Hilo ndilo linalomfanya Yeye kuwa Mungu.

76 Nao walipomwona akija, akipanda kuingia kwenye lango lile, baadhi yao walisema, "Yeye ni Mtu mkuu."

77 Wanasema hivyo siku hizi. Kunazo shule za theolojia zinazofundisha, siku hizi, ya kwamba Yesu alikuwa Mtu mashuhuri, ya kwamba Yeye alikuwa ni Mtu mwema. Baadhi yao hata husema kwamba Yeye alikuwa nabii. Sasa, kama Yeye alikuwa ni nabii tu, ama Mtu mwema, tuko katika dhambi zetu. Alikuwa zaidi ya nabii. Alikuwa zaidi ya Mtu mwema. Hata hivyo, Yeye alikuwa Mtu mwema. Hata hivyo, alikuwa ni Nabii-Mungu. Lakini Yeye alikuwa zaidi ya hayo. Alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, kuondoa dhambi.

78 Na alipokuja, amepanda akiingia ndani, watu wengi walisema, "Yeye ni mponyaji. Loo, tulimwona akiyafungua macho ya vipofu. Tulimwona akimfanya yule kiwete kutembea. Tulimwona akifanya maombi, nayo homa ikamwacha huyo mtoto." Lakini, basi, watu wa aina hiyo walikuwa wakimfuata tu kwa ajili ya mikate na samaki.

79 Na hivyo ndivyo umati wa watu ulivyo siku hizi, wengi. Ikiwa kuna mponyaji, mbona, wao—wao wanamfuata, na Yeye ni—Yeye ni ardhi yenye rutuba na maji tu jangwani. Kama wakiwa wagonjwa, wanakimbia, wanasema, "Loo, utaniombea tafadhali, kwamba Bwana Yesu ataniponya?" Na mara tu wanapotoka hospitalini, ama kwenye kitanda cha wagonjwa, moja kwa moja wanarudi ulimwenguni, kama mbwa kwenye matapiko yake, ama nguruwe kwenye kugaagaa kwake, kama yalivyosema Maandiko. Wanamfuata tu kwa yale mema wanayoweza kupata kutoka Kwake. Wanamtumia tu kama m—mti wa mzimu, au—au kitu ambacho—ambacho wanaweza kupata Kwake, wala hawatarajii kumtumikia. Umati huo ungali unaendelea siku hizi.

80 Kulikuwako na wenye ukoma tisa walioponywa, ndipo mmoja akarudi kumpa sifa. Au walikuwa kumi? Wao, mmoja wao, alirudi kumpa sifa, nao hao wengine wakaenda, bila shukrani.

81 Basi kama watu Marekani, ambao wameponywa kwa Nguvu za Mungu, wangeielekeza mioyo yao kwa Mungu, kungekuwa na uamsho ambao ungelipiga taifa hili ambao ungefunga kila chumba cha kutengenezea pombe haramu, ambao unge...Maduka ya kuuza pombe na maduka ya wiski hayataonekana kabisa. Makanisa yangekuwa yamejaa.

Majumba ya maonyesho yangekuwa matupu Jumapili usiku. Na kungekuwako na uamsho ambao ungetokea, kote katika taifa hili. Lakini wanapoliona likitukia, mambo ambayo Mungu anafanya, wangali wanapiga mayowe, "Yu nani Yeye? Ni nani huyu anayekuja? Walitoka wapi? Ni nani huyu? Hili linafanywa kwa mamlaka gani?"

82 Kamwe sitasahau, huko Johannesburg, Afrika Kusini. Nilikuwa tu nimewasili, yapata dakika thelathini hapo kabla, kwa ndege. Nilikuwa nimekaa angani kwa siku tatu mchana na usiku, nimechoka sana hata ilikuwa vigumu kuvumilia. Wao—wao walinipeleka huko nje kwenye viwanja vya maonyesho ambapo watu wapatao hamsini au sitini elfu walikuwa wamekusanyika. Na mara tu nilipofika jukwaani, Roho Mtakatifu . . . Niliona ba—basi, likipitia mahali pale. Nayo ilikuwa na alama juu yake, "Durban." Nilimwona kijana mmoja ikimbidi kugombana na kuwatoroka baba na mama yake, akiwa na mguu mmoja mfupi kwa inchi sita au nane kuliko huo mwingine. Alikuwa amevaa shati jeupe, huku mikanda imeshikilia suruali yake. Nami nikamwona huyo kijana. Nikatazama nyuma tena. Hilo ono lilikuwa limetoweka. Na halafu, katika muda mfupi tu, nikaiona hiyo Nuru ikining'inia juu ya kijana mmoja, huko nyuma kabisa kwenye wasikilizaji. Nami nikatazama. Nikawazia, "Nilimwona mahali fulani." Nikamwangalia, nayo Nuru hiyo ikaendelea kusimama juu yake kwa dakika chache. Nami nilikuwa nikimngojea mkalimani apate maneno yanayofuata. Ndipo nikamwona kijana yuyo huyo akisimama, akatupa chini magongo yake, na mguu wake mfupi kwa inchi sita ukarefuka ukawa kama huo mwingine.

83 Ndipo nikamwambia Bw. A. J. Schoeman; ambaye yuko Utukufuni, usiku wa leo. Nikasema, "Bw. Schoeman, nukuu tu maneno yangu. Ni ono."

Akasema, "Vizuri sana."

84 Nami nikasema, "Yule kijana anayeketi kule nyuma amevaa shati jeupe, na mikanda, ametoka mji uitwao Durban, kama maili elfu moja mia tano kupitia nchini, kwa basi. Naye ilimbidi kuwatoroka baba na mama yake, kuja. Lakini amemwamini Bwana Yesu, naye ana mguu mmoja mfupi kuliko huo mwingine kwa inchi sita."

85 Ndipo huyo kijana akaruka juu. Huyo hapo, amesimama, akijaribu kushika magongo yake. Kisha nikasema, "Kijana, Bwana Yesu amekuponya." Na mara mguu wake ukarefuka inchi sita, ukafanana, na huo mwingine. Nao wakamleta huyo kijana jukwaani, nao madaktari wakamchunguza pale. Mnaona picha yake kwenye kitabu changu.

86 Nilikuwa nimesimama pale kwa dakika chache tu, nikaona gari dogo, la kijani kibichi likishuka barabarani, nalo likateleza. Likapinduka, kinyumenyume, na kugonga mti. Msichana

mdogo, mwenye nywele za kimanjano alikuwa. . .alikuwa amevunjika mgongo. Nami nikasema, “Ninaona maskini gari la kijani kibichi ambalo liliteleza likagonga mti, naye msichana mwenye nywele za kimanjano mwenye umri wa miaka kumi na minane hivi amevunjika mgongo. Ni mahututi.” Hakuna aliyejibu. Wala nisingeweza kumwona popote katika umati huo mkubwa mno wa watu. Nami nikasimama pale kwa dakika chache tu. Nikasema, “Eleweni. Ni. . .Msiwe na shaka. Ni Bwana Yesu, katika Nguvu za ufufuo. Alimtuma Roho Mtakatifu kuendeleza kazi Yake.” Na hapo nikaona hilo ono likitokea tena. Wala nisingeweza kumwona huyo msichana.

87 Mara, moja kwa moja mbele yangu, ikasimama ile Nuru, kama mnavyoiona kwenye picha. Nayo ikasimama hapa. Nikaenda pale, naye huyo hapo amelala, chini ya jukwaa. Nikasema, “Msichana, Bwana Yesu amekuponya.” Naye akaanza kulia.

88 Mama yake akasema, “Loo, hapana! Usimwambie asimame!” Akasema, “Akijongea, atakufa.”

89 Ndipo huyo msichana akaruka akasimama kwa miguu yake, akipiga mayowe, na kumsifu Mungu. Naye mama yake akazimia na kuanguka kwenye kitanda alichokuwa amelazwa huyo msichana.

Ni kitu gani?

90 Yapata wakati huo tu, mkosoaji fulani akainuka kule nyuma, akasimama huku mguu mmoja uko juu ya kiti kimoja, na mmoja kwa kingine, na kusema, “Ewe, Mmarekani! Nakusahi uniambie ni kwa Jina gani unafanya haya! Na wewe ni wa kanisa gani la kimadhehebu?” Mnaona?

91 Ni vivyo hiyo tu. Hawaelewi. Hawayatazamii mambo haya. Makanisa hayatazamii Kuja kwa Bwana. Naye Roho Mtakatifu yuko hapa kuthibitisha Kuja Kwake, kukutimiza. Sana . . .

Kila mmoja anataka kuchukua njia yake mwenyewe. Hivyo ndivyo ilivyokuwa huko. Kila kundi lilikuwa na wazo lao wenyewe.

92 Lakini hilo silo swali usiku wa leo. Hilo silo ninalozungumzia. Lakini swali ninalowaulizeni, ni, mnafikiri ni kitu gani? Linakuhusu wewe. Ni nani Huyu ambaye anaenda huku na huku katika mataifa? Si watu. Watu hawawezi kufanya mambo hayo. Ni Nani anayezungumza na kuwaambia watu katika kusanyiko, kwamba, “Anayeketi papa *hapa*, upande *huu*,” na sehemu mbalimbali mkutanoni, wakati wanawake na wanaume wanapoletwa humu ndani, wakifa? Ni Nani?

93 Yule msichana aliyeingia mahali pa kubatizia asubuhi ya leo, ambaye majuma matatu yaliyopita, akifa kwa kansa ya kasinoma, anaishi papa hapa kwenye Mtaa wa Maple, Bibi Baity. Nami niliwauliza madaktari watatu waliokuwa pamoja naye.

Hakuwa na nafasi hata moja ya kuishi, akiwa na maskini watoto wanne au watano, na mama yangu akijaribu kuwatunza. Mama alisema, "Bill, kamwe hatarudi nyumbani tena."

94 Nami nikaenda pale alipokuwa, ndipo Bwana Yesu akanena, "BWANA ASEMA HIVI, kama ataenda kanisani na kuahidi kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu, na kumtumikia Mungu, ataenda nyumbani, mzima."

Nami nikamwuliza, "Utafanya hivi, mama?"

95 Naye akasema, "Yote unayosema, nitayafanya." Mara maumivu yakamwacha. Siku tatu baadaye, alikuwa nyumbani, wala madaktari hawawezi kupata dalili hata moja ya kansa hiyo.

96 Ni nani Huyu ajaye kwa Jina la Bwana? Ni Nani? Ni Roho Mtakatifu wa Mungu. Maoni yako kuhusu Hilo ni gani? Maoni yako ni gani, ukimjua mchungaji wako? Na ninapoketi katika viti hivi hapa, watu kutoka nje ya mji, wanaoketi na kifafa, wameketi na . . . Huyu hapa mtu ameketi, mahali fulani humu ndani, ndugu Mmenoni, papa hapa, anayeugua kifafa. Sijawahi kumjua wala kumwona, sijui chochote kumhusu. Na kwa ghafla, yapata miaka miwili iliyopita, nadhani, ama chochote kile, naam, miaka miwili, Roho Mtakatifu alilitaja, na kusema "BWANA ASEMA HIVI." Hajawahi kushikwa na kifafa tangu wakati huo. Ni Nani? Ni Nani?

97 Mwanamke huyu alikuwa ameketi hapa, Jumapili iliyopita, mara ya mwisho nilipokuwa hapa, alikuwa ameshuka kutoka mahali fulani huko Illinois. Kesho yake . . . Akiwa na uvimbe mkubwa mwilini mwake, uliokuwa wa kufisha. Na baadhi ya sayansi bora zaidi ya matibabu ya Illinois ilikuwa ikimpeleka kwenye kliniki kubwa, kufanyiwa upasuaji, Jumatatu. Ndipo akajipenyeza akaingia. Sijapata kumwona wala kusikia habari zake, maishani mwangu mwote. Ndipo ghafla, Roho Mtakatifu akamtia uvuli, Naye akamwambia yeye alikuwa ni nani, alikotoka, naye alikuwa afanyiwe upasuaji kesho yake. Ni wangapi walikuwa hapa wakati huo, kuona jambo hilo? Basi tazama habari zikirudi. Kesho yake, alipoenda kwa daktari, walimpeleka kutoka kliniki hadi nyingine, wala hawawezi kupata dalili yake.

98 Ni nani Huyu? Ee, Mungu uturehemu! Ni nani Huyu anayefanya haya? Je, ungethubutu kusema ilikuwa ni mchungaji wako? La hasha. Ungethubutu kusema watu walikuwa na uhusiano wowote nalo? La hasha. Ni Roho Mtakatifu, Roho aliyekuwa juu ya Bwana wetu Yesu. Na Kuja Kwake kujiunganisha Mwenyewe na Kanisa Lake, kumekaribia sana hata anaitawanya Nuru Yake kuu takatifu, kukomboa, na kuleta katika ushirika, Kanisa la Mungu aliye hai, kwa ajili ya Unyakuo ulio karibu. Amina!

99 Ni Nani? Siwezi kujibu swali lako. Siwezi kukujibia. Lakini naweza kujijibia mwenyewe. Na juu ya dawati hili takatifu, usiku wa leo, kwenye masikio ya hili, hili kundi, na wa—walionunuliwa kwa Damu ya Bwana wetu Yesu, nasema hivi kutoka kwenye kilindi cha moyo wangu. Si kwa sababu mimi ni mmoja wenu, si kwa sababu mimi ni mtu tofauti tu, bali mmoja wa wale waliokombolewa ambao wameoshwa kwa Damu. Ninaamini ya kwamba Nuru iyo hiyo inayoning'inia katika kanisa hili, usiku wa leo, Yuyo huyo anaonyesha, kwa asili Yake, ya kwamba ni Yesu Kristo, katika mfano wa Roho Mtakatifu.

100 Mtu yeyote anayejua Maandiko, anajua kwamba Yesu alisema, "Nilitoka kwa Mungu, tena naenda kwa Mungu." Kabla hajafanyika mwili, wakati akiwa na Musa nyikani, Yeye alikuwa ni Nguzo ya Moto. Ndipo Musa alipotamani kumwona, Yeye alimpitishia mgongo Wake. Ndipo Musa akasema, "Unaonekana kama Mtu." Alipokuwa hapa duniani, Yeye alikuwa ni Mwanadamu. Alifanya mambo yale yale anayofanya, leo hii, kupitia kwa watu ambao amewakomboa. Huyo hapo anakuja na kupigwa picha Yake. Ni kitu gani?

101 Baada ya kifo Chake, kuzikwa na kufufuka, Paulo alikuwa akienda zake Dameski, siku moja, ndipo Nuru kuu ikamwangusha chini. Watu hao waliokuwa karibu naye hawakuiona hiyo Nuru. Lakini ilimwangusha Paulo chini, hata ikampofusha. Alikuwa na shida na macho yake maishani mwake mwote. Naye alisema wakati mmoja, "Makusudi nisipate kujivuna kupita wingi wa hayo mafunuo, nalipewa," mwiba katika mwili wake, mjumbe wa Shetani, ili ampige. Kwa sababu ulikuwa ni wingi wa ufunuo.

102 Na Paulo alipoangushwa chini, akiwa njiani kwenda kuwatesa watu waliokuwa wakipiga kelele nyingi kupita kiasi; kundi lililozaliwa mara ya pili, watu walioitwa wazushi. Paulo alikuwa njiani kwenda kuwatesa hao, akiwa na makaratasi mfukoni mwake, ili kuwakamata na kuwaleta Yerusalemu. Na yapata katikati ya mchana, Nuru ikashuka, ambayo ilimpiga ikamwangusha, chini, naye akaanguka katika mavumbi ya nchi. Ikaja Sauti kutoka kwenye Nuru hiyo, ikisema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

103 Naye Sauli akageuka, katika hali yake ya upofu, akatazama juu. Naye aliweza kuona hiyo Nuru kuu, yenye utukufu. Naye akasema, "Bwana, U Nani Wewe?"

104 Akasema, "Mimi ni Yesu. Nilitoka kwa Mungu; nikaenda kwa Mungu. Ninatoka kwa Mungu; narudi kwa Mungu." Akasema, "Ni vigumu kwako kuupiga teke mchokoo."

105 Ufunuo mmoja juu ya mchanga huo mtakatifu, wakati mmoja juu ya mahali hapo, mtu hawezi kuwa vile vile. Mtu, kabla hajajiita Mkristo, kabla hajaweza kujitambulisha, kwanza

anapaswa kuwa na tukio hilo la upande-wa-nyuma-ya-jangwa, ambapo alikutana na Mungu, uso kwa uso.

106 Kwa kuwa, siku hizi, unaweza kuwa na aina yoyote ya jibu. Unaweza kumwona Bwana akifanya vile hasa Yeye alivyosema ufanye, na wanatheolojia werevu watalielezea vinginevyo. Watasema, "Hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine. Ilikuwa kwa ajili ya *hii*. Ama, ni kwa ajili ya wakati mwingine. Au, ni makosa." Kama walivyosema juu ya Yesu, "Yeye ni Beelzebuli, ibilisi. Yeye ni mpiga ramli." Na mambo hayo yote, wana jibu.

107 Lakini wakati mtu amewahi kamwe kukutana na Kristo, na kumwona kama Paulo alivyomwona, ama kupata tukio Naye, hakuna wanatheolojia wa kutosha ulimwenguni kuweza kuelezea tukio hilo vinginevyo kwa mtu.

108 Hiyo ndiyo sababu, siku hizi, hawana tukio. Hiyo ndiyo sababu hawawezi kusema . . . wote wanasema, "Ni nani Huyu? Ni nini Hii? Inatoka wapi?" Hawana jibu. Kwa nini? Kwa sababu, yote wajuayo ni thiolojia ambayo kanisa fulani limeunda. Sio "kuijua thiolojia" ni Uzima. Sio "kuijua Biblia" ni Uzima.

109 Bali "kumjua Yeye" ni Uzima. "Kumjua Yeye" kama Mwokozi wako binafsi, kama Yule ambaye amekujaza na Uwepo Wake. Ulikuwepo wakati ilipotototendeka. Hakuna mtu anayeweza kuliondoa kwako. Hakuna mtu anayeweza kukuelezea Hilo vinginevyo. Wakati tukio hilo linapokutokea, unajua Yeye ni Nani. Kwangu mimi, Yeye ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

110 Ni nani huyu anayefanya miujiza hii? Ni nani anayefanya kazi hizi kubwa? Je, ni mhubiri? Ni Oral Roberts? Ni Billy Graham? Ni Jack Schuler? William Branham? Yeyote yule, hawana uhusiano wowote nalo. Hao ni vyombo.

111 Ni Roho Mtakatifu akija pamoja na Injili, katika ishara na maajabu na miujiza, kuwatayarisha watu. Hewa imejaa matarajio, huku waaminio wakimtarajia Yeye kuja.

112 Na wengine wanasema, "Kwa nini miamsho hii? Kwa nini tunao? Hebu tutulie kwenye kanisa." Mbona, imesemwa mumu humu kanisani, ya kwamba, tulipoanza kujenga kanisa jipya, kasema, "Hatuhitaji miujiza. Hatuhitaji mambo haya tena. Ukiyataka, nenda huko nje uwanjani ambako yanatokea. Hatuyahitaji hapa." Maskani ya Branham ikiinama kufikia mahali hapo duni, imezama.

113 Kanisa hili limejengwa juu ya kanuni na Nguvu na Injili ya Yesu Kristo. Na maadamu maskani hii imesimama, Roho Mtakatifu mwenye utukufu na apate kuzifikia nafsi, kuokoa, na kujaza na Roho Mtakatifu, na kuponya wagonjwa. Kwangu mimi, ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

Na tuombe.

114 Ikiwa hujui Yeye ni Nani, hujui yote haya yanahusu nini, na ungependa kujua, waweza angalau tu kuinua mkono wako? Na useme, kwa kuinua mkono wako, "Niombee, Ndugu Branham, nipate kumjua." Basi Bwana awabariki. Na pande zote, naiona mikono yenu.

115 Sasa, Baba wa Mbinguni, tunauleta Ujumbe huu, na matunda ya watu wakiinua mikono yao, kwamba wangependa kujua Huyu ni Nani. Wangependa kumfahamu Yesu huyu mkuu. Kwamba, Kuja Kwake, kwa ufufuo, kumekaribia sana, hata wagonjwa wameanza kuponywa. Na baada ya hayo kutukia, ndipo unabii ukaja Kanisani, kisha karama na miujiza, sasa hadi kwenye hiyo ishara ya mwisho. Kitakachofuata, ni Kunyakuliwa, Kanisa litatwaliwa. Na sisi, Bwana, ambao tumedai tunakujua Wewe katika Nguvu za kufufuka Kwako, tunangojea, na kutamani, na kulia, na kusihi, "Njoo, Bwana Yesu!"

116 Linyakue Kanisa Lako na uliondoe, upesi, Bwana. Kwa maana, hivi karibuni, watu watailipua dunia uliyoiumba Wewe wapate kuishi humo, kwa kuwa wamekuasi. Hawajajifunza amani, ila vita. Hawajajifunza haki, bali wamejifunza utundu. Jinsi ambavyo wote hawangekuwa na uchu wa madaraka! Bwana, lile doa dogo moyoni mwao linalowafanya wapate uchu wa madaraka, wanajaribu kuliridhisha katika maabara mahali fulani, kuwalipua wanadamu wenzao.

117 Mungu, laiti wangeweza kutambua ya kwamba nguvu hizo wanazozitamani ni Nguvu za ufufuo wa Mwana wa Mungu, Nguvu za Roho Mtakatifu kuyabadilisha maisha yao; siyo kuyalipua mataifa, bali kuyabadilisha maisha yao na kuwafanya watumishi Wako.

118 Watu wengi, waliopagawa na tamaa mbaya, wanatutambulisha kama kundi la "wasiojua chochote," na—na kama "wazushi," kama walivyofanya katika siku za mwanzoni. Lakini waliporudi, walishangilia, wakikushukuru Wewe ya kwamba wangeweza kustahimili shutuma ya Jina Lako. Hiyo ndiyo hisia ya watoto Wako, usiku wa leo, Bwana, kila mahali. Tuna furaha tu.

119 Wengine katika siku Zako walijaribu kukutambulisha Wewe. Walisema, "Yeye ni rafiki wa yule mtu mshenzi, Yohana, aliyetoka nyikani akiwa karibu uchi, amejizungushia tu maskini ngozi ya kondoo. Mtu mshenzi aliyepayuka maneno, mashariki na magharibi, na kusema, 'Shoka limewekwa kwenye shina la mti.'" Kasema, "Yeye ni m—mfuasi wake. Yeye ni mshenzi. Ana wazimu. Amerukwa na akili." Ile huduma ya kimbinguni iliyokuwa pamoja Nawe, Ee Bwana, iliyapofusha macho ya hao.

120 Na ndivyo imefanya tena siku hizi: Roho huyu Mtakatifu mkuu akikutangulia Kuja kwa Bwana, kama Yohana alivyofanya katika siku zake, akiwapofusha watu, kwa wale wasiotaka

kuona. Lakini kwa wale wanaotaka kuona, Wewe umewachagua. “Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu,” ulisema, “wala hakuna hata mmoja wao atakayepotea. Nami nitamfufua katika siku ya mwisho.” Tunakushukuru kwa jambo hili.

121 Na wale ambao wameinua mikono yao, usiku wa leo, tunaomba, Ee Bwana Mungu, ya kwamba utajitambulisha Mwenyewe kwao, katika tukio, katika Nguvu za ufufuo. Tujalie, Bwana.

122 Na wengine wanaweza kuwa hapa, ambao hawakuinua mkono wao, lakini hata hivyo, moyoni mwao, walijua kwamba walilihitaji. Ninaomba ya kwamba utawabariki, na kuwapa shauku ya moyo wao.

123 Tunapotoka humu jengoni, usiku wa leo, na twende kama watu tofauti. Jalia twende kwa kusudi tofauti na tulilokuwa nalo, tukiingia, kama lilikuwa kinyume na mapenzi Yako ya Kiungu. Na tutoke tukiwa na azimio la kushika pembe za madhabahu, mpaka nafsi yetu imeridhika kwamba tumekuwa na tukio pamoja na Wewe, nasi tunajua ni nani tunayenena habari Zake, kwa sababu tumekutana Naye na tunamjua, na tuna ushirika Naye. Tujalie mambo haya, Baba. Waponye wagonjwa na wanaoteseka.

124 Mbariki mchungaji wetu mpendwa na wa thamani. Mungu, tunaomba ya kwamba Wewe utakuwa pamoja naye na dada zake wapendwa, wanapoimba Injili, na kuihubiri katika redio yao.

125 Wabariki wageni walioko malangoni petu. Bwana, jalia watoke, usiku wa leo, wakiwa na jukumu moyoni mwao, na kusudi kwamba wao, tangu saa hii na kuendelea, ikiwa hawakujui Wewe wala hawajakutumikia, hapo awali, jalia wakutumikie Wewe. Tukijua jambo hili, kwamba, “Mambo mengine yote yatabatilika, bali Neno la Bwana litadumu milele.” Tujalie, Baba.

126 Utusamehe dhambi zetu zote. Na jalia tukutane kwenye ile ninii kuu . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

127 Sasa, baada ya Ujumbe, hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu na kumwabudu, tunapomwimbia.

> Nampenda,

Kwa moyo wako wote.

> Nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

128 Ni wangapi wanampenda kweli? Inua mkono wako, sema hivi kwa ushahidi, "Nampenda." Loo, Yeye si ni wa ajabu? Unajua, ninapenda tu kuketi namna hii na kunywa tu, kwa njia fulani, Uwepo Wake. Neno Lake, limetolewa, limeanguka kwenye mioyo. Linatusahihisha. Linatutiisha chini ya Roho Wake. Jinsi inavyopendeza kumwabudu Yeye basi! Sasa, mnapotoka kanisani, usiku wa leo, nendeni, mkimwabudu Yeye.

129 Pia kumbukeni, juma hili, kuna mkutano wa maombi hapa Jumatano usiku. Msisahau matangazo ya Ndugu Neville Jumapili, au Jumamosi, saa tatu, kwenye WLRP. Ninapenda tu kuwasikiliza, nanyi je? Ule uimbaji wa watu wanne, au watatu, unasikika mzuri sana. Mimi na mke wangu, na watoto, sote huichukua maskini ile redio ndogo na—na kuizunguka, kumsikiliza Ndugu Neville na matangazo yake, na maneno yake ya ajabu, jinsi anavyomtukuza Mungu ambaye anampenda na kumwamini. Usiseme hili kwa . . .

130 Ninyi wageni hapa, kama huna kanisa la nyumbani, njoo ukajiunge nasi. Ninawaambia, sisemi hili naye ameketi hapa. La, bwana. Nimesema hili, mara nyingi. Ninampenda Ndugu Neville. Huyu, kwanza, yeye ni mwanatheolojia. Jambo la kwanza, yeye ni mtoto wa Mungu. Jambo la pili, yeye ni yule yule kila siku. Nimemjua kwa miaka mingi. Hajawahi kubadilika, hata kidogo. Yeye angali ni Orman Neville, mtumishi wa Bwana Yesu. Nami nadhani ana ninii . . .

131 Hivi majuzi usiku, nilipiga simu, kumwomba kama hakuweza, katika mpango wake, angeweza kutupa nafasi ya kushuka kuja na kuwaombea wagonjwa. Kulikuwa na wengine waliokuwa wakiingia, ilikuwa asubuhi ya leo, mwajua. Ndipo maskini mke wake akajibu simu, nami nilikuwa nikizungumza na mke wangu, kule nyuma, kulihusu.

132 Na jinsi tunavyomshukuru Mungu kwa ajili ya maskini mke wake mpendwa na familia yake. Hilo ni zuri sana. Unapomwona mhudumu na mkewe wakipatana namna hiyo, katika utamu na unyenyekevu, hilo hulifanya tu kanisa kujiboresha hata na zaidi. Hilo ni tamu zaidi kadiri siku zinavyosonga mbele.

133 Mnampenda kwa moyo wenu wote? Vema. Tuna wimbo wa kufumukana ambao tunaimba, *Peleka Jina la Yesu*. Na utupe sauti ndogo, dada, kama unao hapo kwenye kitabu. Nasi tutaimba wimbo wetu wa kufumukana. Na tunapoimba kifungu cha kwanza, tunataka kugeuka, tupeane mikono sisi kwa sisi. Vema. Tupe sauti.

> . . . Jina la Yesu,
> Mtoto wa huzuni na majonzi;
> Litakupa furaha na faraja,
> Lipeleke kila uendako.

Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
(Mungu akubariki, ndugu.)
Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Hebu tuchukue kifungu hiki sasa:

Tukiliinamia Jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake,
Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa wafalme,
Safari yetu itakapokamilika. (Hilo si litakuwa zuri sana?)

La thamani...(Jina la thamani!) Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, (Jina la thamani!) Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya...

134 Ni wangapi wanaokumbuka wimbo wetu mdogo tuliokuwa tukiimba, *Usisahau Maombi ya Familia?* Mnaukumbuka? Sininii...Thelma, kama unaujua huo, au sauti, au hujui? Hebu tuujaribu mara moja. Je, huukumbuki? Hebu...Labda ningeweza kuujaribu mara moja pamoja nanyi.

Msisahau maombi ya familia,
Yesu anataka kukutana nanyi pale;
Yeye atachukua kila tatizo lenu,
Loo, msisahu maombi ya familia.

135 Ni wangapi wana maombi ya familia? Hilo ni sawa. Hebu tuujaribu tena. Nitarudisha hicho hapa ndani. Naupenda huo. Sote pamoja sasa:

Usi—usisahau maombi ya familia,
Yesu anataka kukutana nanyi pale;
Yeye atachukua kila tatizo lenu,
Loo, msisahu maombi ya familia.

136 Ee Bwana, imeandikwa katika Maandiko kwamba walitwaa kutoka katika mwili wa Paulo leso au nguo, nao pepo wachafu wakawatoka watu, na magonjwa yakaponywa. Tunaomba, Ee Bwana, ya kwamba vivyo hivyo, itaonyeshwa juu ya hawa, usiku wa leo, ninapozituma kwa wahitaji na wagonjwa. Huko nje mahali fulani nchini, kuna mtu anayetarajia na kungojea hili litendeke. Ninaomba, Baba, ya kwamba utanijalia katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

137 Sasa nitauliza, tunapoinamisha vichwa vyetu, kama Ndugu yetu mpendwa Smith kule, kutoka Church of God, ambaye tumemwona, kama tu Ndugu yetu Neville hapa, kuwa mtumishi mwaminifu, mtiifu wa Mungu, Nitamwomba awaombee baraka,

muendelee katika juma hili lijalo. Mungu awabariki, hata tutakapokutana tena. Ndugu Smith.

[Ndugu Smith anaomba—Mh.] Ndiyo, Bwana. Tujalie, Bwana. Ndiyo. Ndiyo. Ndiyo. Ndiyo. Amina.

138 Peaneni mikono. Karibuni tena, maskanini. Mungu awabariki.

Ni Nani Huyu? SWA59-0510E
(Who Is This?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza kwenye Sikukuu ya Mama, Jumapili jioni, tarehe 10 Mei, 1959, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org